THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
Kenya Certificate of Primary Education

504

# – KISWAHILI –

## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Mar. 2021 – Muda: Saa 1 dakika 40**

### MAAGIZO KWA WATAHINIWA (Soma maagizo yafuatayo kwa makini)

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukiisha kuchagua jibu lako, lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
7. Kwa kila swali 1–50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**
   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **21.** Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.
   A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo.
   B. njuga, tari, kinubi, fidla.
   C. harimuni, marimba, msondo, maleba.
   D. siwa, zeze, upatu, nembo.

   Jibu sahihi ni **B**.

   **Katika karatasi ya majibu:**

   21 [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

for more free material visit www.freekcsepastpapers.com & www.freekcpepastpapers.com

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

© 2020 The Kenya National Examinations Council

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi **1** mpaka **15**. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo **zaidi** kati ya yale uliyopewa.*

Mtu __1__ lugha huanza kwa kutamka sauti za lugha hiyo. Sauti hizo huambatana __2__ kuunda silabi. Neno __3__ kwa idadi maalum ya silabi. Mathalani, neno, 'iliyowambwa' lina silabi __4__. Mtumiaji wa lugha pia hujifunza viambishi vya aina mbalimbali. Kwa mfano, 'ku' katika, 'alikutarajia ufike' inaonyesha __5__. Maneno __6__ ni muhimu katika kuwasiliana. Kwa mfano, neno 'hewala' ambalo ni __7__ huonyesha __8__.

1. A. analojifunza B. anayojifunza C. anaojifunza D. anapojifunza
2. A. ili B. maadamu C. lau D. minajili
3. A. hujengewa B. hujenga C. hujengwa D. hujengea
4. A. 4 B. 5 C. 6 D. 3
5. A. kitenzi B. wakati C. mahali D. nafsi
6. A. nao B. nazo C. nayo D. nako
7. A. kielezi B. kihisishi C. kiunganishi D. kivumishi
8. A. kukubaliana na jambo C. kuomba kitu kisimuumize mtu
   B. kuajabia kitu unachoona D. kueleza jinsi jambo litendakavyo

Lugha __9__ mazingira anamoishi binadamu. Huwa na misamiati mbalimbali. __10__ misamiati hii ni ya uhunzi kama vile kusana. Isitoshe, mwanafunzi hujifunza kuunda neno kutokana na __11__. Kutokana na nomino 'mtu' tunapata nomino 'utu' ilhali kivumishi 'nyepesi' huunda nomino __12__. Mwanafunzi huandika sentensi katika kauli tofautitofauti. Sentensi, 'Afisa alikagua cheti cha Hamu' katika kauli ya kutendea ni __13__. Ushairi pia ni kipengele cha lugha __14__ huwachangamsha wanafunzi. Mashairi kama vile __15__ huwa na mishororo mitano katika kila ubeti.

9. A. huelezeka B. huelezwa C. huelezewa D. huelezea
10. A. Mbali na B. Baadhi ya C. Mkabala na D. Zaidi ya
11. A. nyingine B. lingine C. mwingine D. kwingine
12. A. jepesi B. upesi C. wepesi D. mwepesi
13. A. Afisa alikagulia cheti kwa Hamu B. Cheti kilikaguliwa Hamu na Afisa
    C. Cheti kilikaguliwa Hamu kwa Afisa D. Afisa alimkagulia Hamu cheti
14. A. ambacho B. ambao C. ambayo D. ambalo
15. A. tathnia B. tathlitha C. takhmisa D. tasdisa

for more free material visit www.freekcsepastpapers.com & www.freekcsepastpapers.com

*Kutoka swali la **16** mpaka **30**, chagua jibu sahihi.*

**16.** Chagua wingi wa: Chifu atamwongoza kushughulikia jambo hilo kijijini.
A. Chifu atawaongoza kushughulikia jambo hilo vijijini.
B. Chifu atawaongoza kushughulikia mambo hayo vijijini.
C. Machifu watawaongoza kushughulikia mambo hayo vijijini.
D. Machifu watawaongoza kushughulikia jambo hilo vijijini.

**17.** Ni sentensi ipi iliyotumia 'na' kama kiunganishi?
A. Uchumi utaimarishwa na wananchi wote.
B. Ukumbi huo una waigizaji wengi.
C. Hao wanaandikiwa barua kutoka ughaibuni.
D. Amosi aliwapikia na kuwapakulia chakula hicho.

**18.** Chagua kitenzi chenye kiwakilishi '**wa**' cha mtenda.
A. watamchezea
B. aliwakaribisha
C. tuliwahimiza
D. uliwasomeshea

**19.** Ni sentensi ipi iliyotumia wakati uliopita hali timilifu?
A. Ngao hii itakuwa imetumika kabla ya mashindano ya mwakani.
B. Ngoma ile ilikuwa imepasuliwa baada ya wachezaji kupumzika.
C. Nguo yake ilikuwa inanunuliwa kabla ya sherehe hiyo.
D. Nyumba yao itakuwa inajengwa baada ya kubomolewa.

**20.** Chagua ukanushaji wa sentensi ifuatayo: Mwale ananunua kanga akizipanga kwenye sanduku.
A. Mwale hajanunua kanga akizipangi kwenye sanduku.
B. Mwale hakununua kanga akizipanga kwenye sanduku.
C. Mwale hatanunua kanga akizipanga kwenye sanduku.
D. Mwale hanunui kanga akizipanga kwenye sanduku.

**21.** Onyesha jibu lenye maneno ambayo **si visawe**.
A. giza – mwangaza
B. vizuri – vyema
C. kidole – chanda
D. fika – wasili

**22.** Ni sentensi ipi yenye kivumishi cha pekee?
A. Mti huu ni mrefu ukilinganishwa na ule.
B. Kijana mtiifu atatuzwa na mlezi wake.
C. Jembe lenyewe limevunjika mpini.
D. Nchi inahitaji askari wengi kudumisha usalama.

**23.** Chagua jibu **lisilotumia** maneno ya adabu.
A. Mweke alihitaji kujisaidia kabla ya kuanza safari.
B. Juma atakuwa amekula chumvi nyingi katika umri huo.
C. Mtoto akihara na kukojoa damu huwa hatarini.
D. Kinyesi cha ndovu huwaelekeza watalii kwa kupitia.

**24.** Mjomba ni kwa shangazi ilhali buda ni kwa:
A. kigoli
B. ajuza
C. ghulamu
D. shaibu

**25.** Onyesha jibu **lisiloambatanishwa** ipasavyo.
A. Ridhaa – malipo ambayo mtu hupewa kwa kuokota kitu
B. Fidia – malipo anayopewa mtu aliyefikwa na hasara
C. Kiingilio – malipo anayotoa mtu kutazama mchezo uwanjani
D. Faini – malipo anayotozwa mtu aliyepatikana na hatia.

**26.** Akisami $\frac{5}{6}$ kwa maneno ni:
A. subui tano
B. tusui tano
C. thumni tano
D. sudusi tano

**27.** Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.
A. Kaari ni bintiye shem: Kaari pia ni mwalimu.
B. "Kesi hii" akasema jaji itaamuliwa kesho."
C. Nyimbo – nyingi zile za zamani – zinawavutia wengi.
D. Mashi (yule kijana aliyefuzu juzi) amekiletea kijiji hiki fahari.

**28.** Kidani ni kwa shingo ilhali ________ ni kwa mkono.
A. kikuku
B. hazama
C. kikuba
D. njuga

**29.** Konga ni kuzeeka, konga pia ni ___________
A. kutumia mrija kuvuta kinywaji baridi.
B. kuleta watu pamoja kwa shughuli fulani.
C. kupunguza hamu ya kitu usicho nacho.
D. kukubaliana na jambo ambalo wengine wamelijadili.

**30.** Kauli iliyopigiwa mstari imetumia tamathali gani ya usemi?

Matone makali ya mvua <u>**yaliusalimia**</u> uso wake.
A. nahau
B. sitiari
C. ishara
D. tashhisi

For more free materials visit www.freekcsepastpapers.com & www.freekcsepastpapers.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **31** mpaka **40**.*

Bila shaka umewahi kushiriki katika michezo mbalimbali shuleni au kijijini. Hata hivyo, nikikuuliza kuhusu umuhimu wa michezo hiyo katika maisha yako huenda ukachukua sekunde moja au mbili kujibu. Kwa nini hali iwe hivyo? Ni kwa sababu upo wakati katika maisha yetu ya utoto na hata ya utu uzima ambao tunashiriki shughuli fulani kabla ya kuipa fikira ifaayo. Wakati mwingine tunajipata tukiuma vidole: tumejiponza kwa uamuzi wetu.

Sijui unajihisi vipi wakati ambapo unashiriki na wenzako katika michezo kama vile kibe au mwajificho. Je, wakati ambapo unajificha nyuma ya mlango wa sebule, mnuna au mlungizi wako akutafute kwa udi na uvumba asikupate, unahisi vipi? Si, unajihisi kuwa shujaa au bingwa? Je, hili linakupa hamu zaidi ya kutafuta mikakati bora ya kujificha ili nao watafute mbinu bora zaidi za kukutafuta? Je, wakati unawasikiliza kutoka mafichoni wakikuita, "Mweledi, tafadhali jitokeze," si unaingiwa na fahari kwa kuwa mshindi?" Hivyo ndivyo tulivyohisi tulipocheza kibe zamani.

Yumkini umewahi kurusha tiara kwenye uwanja wa shule. Huu ni mchezo ambao tuliupenda sana tukiwa watoto. Nakumbuka wakati huo ningesimama katikati ya uwanja mkubwa wa michezo kijijini mwetu. Ningeishika tiara yangu na kuitupa juu, naiamrisha ipae. Tiara ingepaa kwa mbwembwe juu huko mbinguni, inafika kileleni mwa mbingu jinsi kipungu afanyavyo. Katika hali hii, licha ya kuburudika, ningejihisi kana kwamba naumiliki ulimwengu mzima; nimeweza kuyadhibiti maisha yangu na kukidhibiti chombo chenyewe. Najua pia umewahi kushiriki katika michezo mingine ya watoto kama nilivyofanya. Kumbuka ulivyojifanya wewe ni mama, unawapikia na kuwafumia fulana watoto wako! Kumbuka ulivyoona fahari wenzako walipokuita mama, nawe unawahimiza kuwa na nidhamu; wakati mwingine hata unamwigiza mzazi wako kwa kuwapiga! Najua nikikuuliza utaniambia kwamba michezo kama hii ilikusaidia kupalilia kipawa chako cha uigizaji. Haitakuwa ajabu ukiniambia kuwa hivi sasa wewe ni mwigizaji mahiri katika shule yako.

Ikiwa ulikulia katika kijiji ambamo familia zilijenga karibu karibu, utakumbuka jinsi aghalabu mlivyokusanyika kila mchana na hata jioni kupitisha muda. Sijui kama uliwahi kushiriki katika vikao vya kushindana utamkaji wa vitanza ndimi, kutega na kutegua vitendawili, na hata kutambiana hadithi. Ni dhahiri kwamba, licha ya vikao hivi kuwaleta pamoja kama wanakijiji, viliwachangamsha na kunoa bongo zenu. Najua utaniambia kuwa vikao hivi viliibua ucheshi mkubwa. Kumbuka namna ulivyomcheka mwenzako wakati alipotamka vibaya, naye akakukumbusha jinsi ulivyoshindwa kuruka kamba katika mchezo wa kuruka kamba!

Ni wazi kwamba michezo ina manufaa makubwa kwako. Ukipigia darubini maisha yako ya utotoni, utakumbuka ule mchezo wa kuketi katika duara huku mmoja wenu akikimbia kuzunguka duara hiyo na kumpokeza mmoja wenu zamu yake kukimbia kwa kumpiga kwa kitambaa fulani begani au hata kichwani. Mbio hizi si tofauti na zile wanazoshiriki wakimbiaji hodari nchini. Pamoja na kunyoosha misuli na kupumzisha akili, mbio hizi huimarisha afya ya anayeshiriki. Yeye kila mara hujihisi mwepesi kama unyoya. Chakula anachokula hutumika vyema mwilini, hivyo kukinga dhidi ya kujinenepea ovyo.

Usidhani ni mbio tu ambazo ni muhimu. Ipo michezo mingine kama vile uogeleaji na kandanda. Nakumbuka kijijini tuliogelea na kupiga kachombe kwenye vidimbwi na mabwawa ya kiasili. Siku hizi mmejengewa mabwawa maalumu. Wachezaji wa michezo kama hii hupata umaarufu kitaifa na kimataifa. Hali kadhalika, wachezaji wengi wameweza kujiendeleza kiuchumi kutokana na fedha wanazopata kutoka michezoni. Wengine hujipatia marafiki wa kudumu kupitia michezo hii. Wapo hata waliowahi kufunga ndoa na waja kutoka mataifa mengine!

Ni muhimu kukumbuka kwamba ule wakati ambao michezo ilihusishwa na watu wasiojiweza kimasomo **umetupa kisogo**. Ni muhimu kuanza kutambua na kuvitumia vipawa vyetu kwa njia ifaayo. Wale walio na vipawa katika michezo nao watahadhari dhidi ya kuchukua muda wao wote katika mchezo na kuyapuuza masomo. Elimu ndiyo itakayokuwezesha kutumia mtaji unaopata michezoni kwa njia inayokufaidi wewe na jamii yako.

**31.** Katika aya ya **kwanza** mwandishi:

A. Awaza kuwa msomaji atakuwa mwanamichezo kijijini.
B. Ana hakika kwamba msomaji aliwahi kucheza.
C. Ana tumaini kwamba msomaji anaweza kucheza.
D. Anajua kwamba msomaji alichezea shule.

**32.** Aya ya **kwanza** inaonyesha hali ya watu:

A. Kufanya mambo yasiyo na faida kwao.
B. Kutotambua lengo la michezo shuleni.
C. Kutozingatia ubora wa kuepuka majuto.
D. Kujihusisha na shughuli bila kuwazia maana yake.

**33.** Kulingana na aya ya **pili,** Kibe:

A. Humpa mtu hamu ya kushirikiana na familia.
B. Hurahisisha juhudi za kuwatafutia wengine suluhisho.
C. Humfanya mtu kufahamu jinsi wengine wanavyohepa.
D. Humwezesha mtu kujivunia uwezo wake katika jambo.

**34.** Mwandishi:

A. Alijithamini zaidi kwa kufahamu kufanana kwa uwezo wa tiara na wa kipungu.
B. Alijiamini zaidi kwa kutambua amechangia katika mafanikio yake.
C. Alijasirika zaidi kwa kung'amua kwamba amehusika katika kuiboresha dunia.
D. Alipumbazika zaidi kwa kufikia mbingu wakiwa watoto.

**35.** Chagua jibu ambalo **si sahihi** kulingana na aya ya **tatu**.

A. Mtu anapoiga yafanywayo na wengine huwa na mafanikio mengi shuleni.
B. Wanajamii wanaweza kurekebisha tabia hata katika shughuli za kawaida.
C. Tuyafanyayo tukiwa watoto baadaye huathiri mazoea yetu.
D. kufanikiwa katika jambo ni njia ya kujenga tabia.

**36.** Kifungu kimeonyesha kwamba, ilikuwa kawaida kwa:

A. Nyumba kuwa karibu na nyingine.
B. Makundi kuandikiana vitanza ndimi.
C. Watoto kujumuika pamoja katika shughuli.
D. Vikao kukumbushana kuhusu kushindwa.

**37.** Chagua umuhimu wa michezo kwa mujibu wa aya ya **nne.**

A. Huleta ubunifu, hustawisha utani.
B. Huimarisha utamkaji wa sauti, huboresha uwazaji.
C. Hukuza ushirikiano wa kijamii, huokoa wakati.
D. Huliwaza washiriki, huwatumbuiza wanaosimulia hadithi.

**38.** Kwa mujibu wa kifungu:

A. Michezo husaidia mwili kunufaika kwa lishe upatayo.
B. Mbio za kuzunguka huifanya akili ya mtu kufikiri vyema.
C. Urafiki wa dhati hupatikana baada ya michezo.
D. Waogeleaji hupata sifa wanapoogelea ng'ambo.

**39.** Kulingana na aya ya mwisho elimu:

A. Humpa mtu stadi za kutumia alichofanikiwa na kuinua jamii.
B. Humpa mtu fursa ya kujua namna ya kupanga wakati ili kuimarisha utendakazi.
C. Humwezesha mtu kufahamu nafasi aliyo nayo.
D. Humwezesha mtu kutambua faida ya vipawa.

**40.** Maana ya **umetupa kisogo** ni

A. Umepuuzwa
B. Umesahaulika
C. Umepita
D. Umebadilika

for more free material visit www.freekcsepastpapers.com & www.freekcsepastpapers.com

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Baridi na mzizimo vilishindana kuipiga pambaja ngozi yangu laini. Nilitazama huku na huko kuona iwapo nitamwona binadamu yeyote niliyemfahamu katika uwanja huu wa ndege ulioshiba ukatapika watu na shughuli. Woga wa ajabu ulinikumbatia. Moyo wangu ulianza kunidhihaki na kunihukumu kwa kuiacha nchi na watu niliowajua na kujitoma katika ulimwengu wenye kadhia nisizokuwa na mwao nazo.

Hata nilipokuwa natunga macho mbele kuona iwapo mwajiri wangu huyu atawasili, **maswali kikwi yaliivamia akili yangu.** "Kipi kilichokufanya kuiacha familia yako ukiwa mkembe na kuukimbilia mji? Je, ungekaa kijijini mwako Mama Kedi angekutuma huku ughaibuni kuja kumfanyia kazi binadamu usiyehusiana naye kwa damu wala usaha?" Hapo hapo nilijipurukusha kuyajibu maswali haya akilini mwangu, nikayarudisha mawazo yangu nyuma na kuileta picha ya maisha yangu mbele ya macho yangu.

Nilikumbuka asubuhi moja mbichi katika kijiji chetu cha Tugawane. Siku moja niliwaona wazee watatu wamewasili kwetu. Ilikuwa siku ya tano baada ya mazishi ya mama yangu ambaye ndiye mzazi wa pekee niliyemfahamu. Baba yangu nasikia alikuwa amefariki miaka minne kabla ya kifo cha mama kwa ugonjwa ule ule uliomuua mama. Wazee hawa waliniambia kuwa mimi na mnuna wangu tulikuwa mayatima, hivyo tulihitajika kwenda kulelewa na mmoja kati ya ndugu za baba. Nilijaribu kupinga, nikisema kwamba tungeweza kuishi katika nyumba ya wazazi wangu tukitunzwa na dada yake baba lakini wakakataa katakata.

Nakumbuka jinsi mimi na ndugu yangu Tunu tulivyokumbatiana, machozi ya ukiwa yakitiririka. Tulikusanya virago vyetu na kuondoka; kila mmoja anaelekea njia yake. Mimi niliandamana na baba mdogo, naye ndugu yangu na baba mkubwa. Maisha kwa baba mdogo yalikuwa kama ya mtoto mdogo aliyekosa titi la mama na kulazimika kuamwa la mbwa. Vicheko nilivyokuwa nimezoea kwetu viliyeyuka. Kwa baba mdogo hakukuwa na nafasi ya wasichana kwenda shule. Walilelewa ili wakipevuka kidogo waozwe kwa wazee ambao walikuwa tayari kutoa fungu kubwa la mahari. Binamu zangu hawakujali wala kupinga hali hii. Hata hivyo, mimi binafsi niliishi kwa hamaniko kuu. Nilimwomba Mungu kila mara asinijalie kukua. **Ingawa sikudiriki kuhudhuria shule nikiwa kwa baba mdogo niliiona hali hii kuwa bora kuliko kuozwa kwa mzee.**

Jioni moja ya kipupwe ilishuhudia mabadiliko makubwa katika maisha yangu. Jioni hiyo nilimsikia baba mkubwa na baba mdogo wakijadiliana kuhusu namna walivyogawana mashamba na mali ya wazazi wetu. Lililonishtua zaidi ni kusikia baba mdogo akisema kwamba tayari pametokea mzee ambaye amekuja kuniposa. Usiku huo huo niliamua kuwa kwa baba mdogo hakuniweki tena. Alfajiri na mapema ilinipata kwenye baraste kuu, nikiabiri matwana kutokomea jijini. Ya ndugu yangu mdogo siyajui hadi sasa.

Msomaji, hata ninapokuhadithia haya, machozi yananitiririka nikikumbuka namna nilivyojitoma kwenye mitaa ya jiji na kuanza kung'ang'ania makombo kwenye majaa na watoto wengine ambao walidai kuwa waliondoka kwao baada ya kuchoshwa na sheria kali za wazazi wao. Msomaji, sikwambii ni siku ngapi nililala njaa, na ngapi niliuweka ubavu kwenye vijia vilivyokuwa katikati ya majengo, **roho mkononi** nikichelea kutendewa unyama. Hali hii, pamoja na kutokuwa na msukumo wa kurudi nyuma nilikotoka ndizo zilizonisukuma kulikubali ombi la Bi Kedi la kunisafirisha mimi na wasichana wengine watano kufanya kazi kama vijakazi katika nchi hii ambayo imebaidika na kwetu kama ardhi na mbingu. Siijui vipi mtoto wa umri wa miaka kumi na mitano anatarajiwa kuimudu kazi hii. Lakini ni maji ambayo nimeyavulia nguo.

for more free material visit www.freekcsepastpapers.com & www.freekcpepastpapers.com

41. Kulingana na aya ya **kwanza:**

A. Msimulizi alijuta kwa sababu hakukutana na amjuaye.
B. Hali ngeni iliyomzunguka Msimulizi ilimtia wasiwasi.
C. Nchi aliyohamia ina matukio yaliyomshangaza Msimulizi.
D. Shughuli nyingi uwanjani zilimtia huzuni Msimulizi.

42. Aya ya **tatu** imebainisha kwamba:

A. Msimulizi hakujua habari za baba yake.
B. Walio na mayatima walijitolea kumlea Msimulizi na nduguye.
C. Msimulizi alihofia kulelewa na ami zake.
D. Dada yake baba aliwalea vyema Msimulizi na ndugu yake.

43. Chagua athari za uyatima kwa mujibu wa kufungu.

A. Kutengana na familia, kudhoofika kwa malezi.
B. Wasiwasi, udanganyifu.
C. Kusafiri nchi jirani, kubaguliwa shuleni.
D. Umaskini, kujidharau.

44. Chagua jibu ambalo **si sahihi** kulingana na aya ya **nne**.

A. Baba mdogo alimnyima Msimulizi mengi aliyoyapata kwao.
B. Wasichana waliokomaa ndio waliohitaji mahari nyingi.
C. Watoto wa baba mdogo waliridhika na hali yao.
D. Jamii ya Msimulizi inaendeleza ubaguzi wa kijinsia.

45. **Ingawa sikudiriki kuhudhuria shule nikiwa kwa baba mdogo, niliiona hali hii kuwa bora kuliko kuozwa kwa mzee.** Andika methali inayoweza kujumuisha ujumbe wa maneno haya.

A. Mwacha kiwi hanacho na chema kimpotele.
B. Kenda fumbata si kumi nenda rudi.
C. Heri nusu ya shari kuliko shari kamili.
D. Bura yangu sibadili na rehani.

46. Kwa nini **hasa** ami za Msimulizi walitaka kuwalea? Waliongozwa na

A. tamaa ya kumiliki mali ya wazazi wa Msimulizi
B. hamu ya kujua urithi wa wazazi wa Msimulizi
C. haja ya kupata mahari baada ya binti kuozwa
D. tumaini la kufaidi kwa watoto wakimaliza shule.

47. Chagua changamoto zinazowakabili watoto wa mitaani kulingana na aya ya mwisho.

A. Uhaba wa chakula, kutopata washirika.
B. Kudhibitiwa na wazazi, kushindana kwenye majaa.
C. Malazi duni, kutafuta walezi.
D. Ukosefu wa usalama, kunyanyaswa kimapenzi.

48. Kulingana na aya ya mwisho:

A. Mazingira duni ya mjini yalimfanya Bi Kedi aanzishe biashara ya vijakazi.
B. Kuwachukia wasichana kuliwafanya kukubali kuwa vijakazi.
C. Msimulizi yu tayari kukabiliana na hali ngumu anayotazamia.
D. Umri unamfanya Msimulizi kuogopa ng'ambo.

49. Kauli, '**maswali kikwi yaliivamia akili yangu**' imetumia tamathali gani ya usemi?

A. Nahau.
B. Tashihisi.
C. Sitiari.
D. Majazi.

50. Kuwa **roho mkononi** ni:

A. Kupata hisia tele.
B. Kuonyesha tuhuma kuu.
C. Kuwa na woga mwingi.
D. Kujawa na huzuni nyingi.

For more free material visit www.freekcsepastpapers.com & www.freekcsepastpapers.com